



ARUSHA MEAT COMPANY LTD

P. O. BOX 14167

ARUSHA

TANZANIA

E-mail: arushameatcompany@yahoo.com

TEL: +255 272970304

Mob: +255734026767

KUMB. NA. AMCO/STF/010/36

DATE:04/11 /2022.

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Arusha Meat Company Limited ni Kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria za Makampuni ndani ya Jamuhuri ya Muungano kwa kujishughulisha na huduma ya uchinjaji wa ng'ombe, mbuzi na kondoo. Aidha Kampuni hii pia huchakata nyama kwa ajili ya kutengeneza bidhaa mbalimbali. Arusha Meat Company Limited inakaribisha waombaji wenyewe sifa kujaza nafasi iliyowazi kama ifuatavyo:

1.0. AFISA MANUNUZI NA UGAVI II (PROCUREMENT OFFICER II) NAFASI MOJA (1).

1.1. MAJUKUMU YATAKUWA KAMA IFUATAVYO:

- 1) Kukusanya takwimu za kusaidia kutayarisha makisio ya vifaa vinavyohitajika na mpango wa manunuizi (Procurement Plan) ndani ya Kampuni.
- 2) Kukusanya na kutunza takwimu za wazabuni.
- 3) Kukusanya na kutunza takwimu za upokeaji, utunzaji na usambazaji wa vifaa katika Kampuni.
- 4) Kusimamia utunzaji wa maghala (Store).
- 5) Kupokea, kutunza na kusambaza vifaa (Physical distribution).
- 6) Kubuni mfumo wa uwekaji na utunzaji wa vifaa ghalani (Location index design).
- 7) Kukagua na kuhesabu vifaa ghalani (Perpetual Stock Checking).
- 8) Kutayarisha mpango wa kazi katika vipindi maalum.
- 9) Kuhesabu na kutoa taarifa ya thamani ya vifaa vilivymo ghalani kila robo ya mwisho wa mwaka (Quarterly Stock Taking).

- 10) Kusimamia manunuizi, utunzaji na matumizi bora ya vifaa vya kazi katika Kampuni.
- 11) Kuandaa hati ya kupokelea vifaa.
- 12) Kumshauri na kumsaidia Meneja ugavi katika masuala yote yahusuyo manunuizi.
- 13) Kuandaa na kuititia orodha ya mahitaji.
- 14) Kutunza kumbukumbu za manunuizi.
- 15) Kusaidia majukumu ya Bodi ya zabuni.
- 16) Kutekeleza maamuzi ya Bodi ya Zabuni.
- 17) Kutoa mikataba ya wazabuni iliyokwisha kusainiwa.
- 18) Kuandaa mikataba ya wazabuni.
- 19) Kuandaa taarifa ya Robo ya bodi ya zabuni.
- 20) Kufanya jukumu lolote lile atakalopangiwa na mwajiri.

SIFA ZA MWOMBAJI.

- a) Awe na Shahada katika Manunuizi na Ugavi (Bachelor Degree in Procurement and Supply) au Stashahada ya juu ya Ugavi (Advanced Diploma in Material Management) inayotolewa na Chuo kinachotambuliwa na Serikali.
- b) Mwenye cheti cha taaluma kutoka Bodi ya Manunuizi atapewa kipaumbele.
- c) Mwenye uzoefu usiopungua Miaka miwili (**2**) katika fani hiyo atapewa kipaumbele.
- d) Awe na uwezo wa kufanya kazi katika mazingira yenye kazi nyingi na kuzikamilisha bila kuathiri matokeo.
- e) Awe na ujuzi wa kutumia Kompyuta.

1.2. MSHAHARA:

Kwa kuzingatia ngazi za Mishahara ya Arusha Meat Co. Ltd yaani ngazi ya **AMC 7.**

MASHARTI YA JUMLA KWA NAFASI ILIYOTANGAZWA.

- i. Waombaji wawe raia wa Tanzania.
- ii. Waombaji waambatanishe Cheti cha kuzaliwa.
- iii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu pamoja na barua ilyoandikwa kwa mkono na kusainiwa.
- iv. Anuani na namba ya simu ya mwombaji na picha moja "Passport size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.
- v. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, nakala za vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika vyeti vya kitaaluma (professional certificate) kutoka bodi husika na viwe "Certified".
- vi. "Testimonials" "provisional results" "statement of result" hati matokeo za kidato cha nne na sita **HAVITAKUBALIWA**.
- vii. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika (TCU, NECTA, NACTE).
- viii. Mwombaji atajigharamia mwenyewe wakati wa usaili.
- ix. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili **HAYATAPOKELEWA**.
- x. Ajira hii ni ya mkataba wa muda maalum.

NB: Barua zote za maombi zitumwe kwa njia ya Posta kwa anuani ifuatayo:

MENEJA MKUU,
ARUSHA MEAT CO. LTD,
S.L.P 14167,
ARUSHA-TANZANIA.

NB: Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **17/11/2022**.

Imetolewa na: -

STEPHEN L. SULTAN
MENEJA MKUU
ARUSHA MEAT CO. LTD

Nakala:

- Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi (AMCL),
S.L.P 14167,
ARUSHA.
- Mbao za matangazo.
- Tovuti ya Kampuni.